AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**KIJA NESTORY DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 015/2018**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 NOVEMBA 2024**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha , tarehe 13 Novemba 2024**, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa hukumu katika kesi ya *Kija Nestory dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Kija Nestory (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye, wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Uyui, akisubiri kutekelezwa kwa hukumu ya kifo, baada ya kupatikana na hatia ya kosa la mauaji. Alidai kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi), ilikiuka haki zake za kusikilizwa kwa haki kutokana na jinsi mahakama iliyosikiliza kesi yake na ilivyotoa hukumu yake.

Mjibu Maombi hakuwasilisha utetezi katika Maombi haya. Kwa hivyo, Mahakama ilitoa hukumu moja kwa moja katika kesi hii baada ya kuzingatia matakwa ya kutoa hukumu moja kwa moja kama ilivyoainishwa chini ya Kanuni ya 63 (1) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama iliridhika kwamba masharti mawili kwamba, Mjibu Maombi alikuwa amepewa hati zote zinazohusiana na kesi; na kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekosea kwa kushindwa kuwasilisha Majibu yake yalikuwa yametimizwa.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), Mahakama iliona kwamba ilipaswa kwanza kuamua endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Maombi haya kuwasilishwa, mnamo tarehe 6 Desemba 2018.

Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kisheria kwa sababu Mleta Maombi alikuwa amedai haki zake, zinazolindwa chini ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) zilikiukwa. Aidha, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Kuhusu ukubalifu, Mjibu Maombi hakutoa pingamizi lolote kuhusu ukubalifu wa Maombi haya. Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, ambacho maudhui yake yamerudiwa katika Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Kwa hivyo, Mahakama iliangalia endapo maombi yalizingatia matakwa yote ya ukubalifu yaliyowekwa chini ya Kifungu cha 56 cha Mkataba na kama pia ilivyoelezwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama yalitimizwa.

Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi ametambuliwa dhahiri kwa jina kama ilivyoelezwa chini ya Kanuni ya 50(2)(a); Maombi haya hayakuwa na madai au maombi yoyote ambayo hayakuafikiana na masharti ya Sheria ya Katiba ya Umoja wa Afrika na Mkataba kama ilivyoelezwa chini ya Kanuni ya 50(2)(b); Lugha iliyotumiwa katika Maombi haikuwa ya kudharau au kumtukana Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c); Maombi hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, kwani yalitokana na nyaraka za mahakama kutoka mahakama za ndani za Mjibu Maombi, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d); Matakwa ya kukamilisha taratibu zote za ndani yametimizwa kwa mujibu wa Kanuni ya 50(2)(e), kwa kuwa Mleta Maombi alikuwa ametumia katika ngazi ya ndani hadi Mahakama ya Rufaa, mahakama ya juu zaidi ya Mjibu Maombi. Aidha, Mahakama ilizingatia kwamba Maombi yalikuwa yamewasilishwa mbele yake, ndani ya muda unaofaa kabisa, wa miezi tisa (9) na siku tisa (9) baada ya kukamilisha taratibu za ndani katika kutimiza matakwa ya Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Katika suala hili, pia ilibainisha kuwa hapo awali iliona kwamba ndani ya mfumo wa mahakama wa Mjibu Maombi, utaratibu wa Mahakama ya Rufaa kupitia upya uamuzi wake ni njia isiyo ya kawaida ambayo Waleta Maombi hawahitajiki kukamilisha kabla ya kuwasilisha Maombi yao mbele ya Mahakama hii; na mwisho, ilibaini kwamba Maombi haya hayakuhusu kesi ambayo tayari imesuluhishwa na Wahusika kwa mujibu wa kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa, Sheria ya Katiba ya Umoja wa Afrika, masharti ya Mkataba na yalizingatia Kanuni ya 50(2)(g). Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Maombi haya yalikuwa yamekidhi matakwa yote ya ukubalifu na ikaamua kuwa yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria, Mahakama iliangalia ukiukaji unaodaiwa kufanywa kwamba katika kufikia hitimisho la hukumu yake kulingana na kanuni ya umiliki wa hivi karibuni, Mjibu Maombi alitegemea ushahidi wa kimazingira, ambao ulikuwa dhaifu, unaoishia kwenye tuhuma tu na haukuthibitishwa pasipo shaka yoyote, na kusababisha ukiukaji wa haki yake ya kusikilizwa kwa haki. Mahakama hii ilibaini kwamba Mleta Maombi alikuwa ameshindwa kuonyesha jinsi alivyohukumiwa kwa msingi wa ushahidi ambao

haukuthibitishwa kuwa na shaka yoyote. Pia ilibaini kwamba Mahakama Kuu ilizingatia kikamilifu ushahidi uliowasilishwa katika kesi ya Mleta Maombi na matokeo yake yalithibitishwa na Mahakama ya Rufaa. Kwa hivyo, iligundua kwamba Mjibu Maombi hakukiuka haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki.

Ingawa Mleta Maombi hakudai waziwazi kwamba alihukumiwa kifo kwa lazima kwa kosa la mauaji na kwamba haki yake ya utu ilikiukwa, Mahakama iliamua kwa busara yake kufanya uamuzi ikiwa matokeo katika suala hili yalikuwa sahihi, ikizingatiwa kuwa hapo awali ilikuwa imeamua juu ya masuala haya.

Ilitokana na kumbukumbu kwamba Mleta Maombi alihukumiwa kifo kwa cha lazima chini ya sheria ambayo hairuhusu uamuzi wa afisa wa mahakama kutoa adhabu tofauti. Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria, ambayo ilibainisha kuwa kutolewa kwa adhabu ya lazima ya kifo ni ukiukaji wa haki ya kuishi kama ilivyohakikishwa chini ya Mkataba. Kwa hivyo iliona kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka Kifungu cha 4 cha Mkataba kuhusu haki ya kuishi.

Kuhusu ukiukaji wa haki ya utu ya Mleta Maombi chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba, kulingana na kumbukumbu, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alihukumiwa kifo kwa kunyongwa. Vivyo hivyo, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba kunyongwa kama njia ya kutekeleza adhabu ya kifo kulihusisha maumivu makubwa na yasiyo ya lazima na kwa hivyo ilikuwa ya kikatili, ya kinyama, na ya kudhalilisha. Kwa hivyo Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki ya utu ya Mleta Maombi kwa kutoa hukumu ya kifo kwa kunyongwa.

Kuhusu fidia, kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Itifaki, Mahakama ilirejelea kwamba ikiwa itabaini kuwa kumekuwa na ukiukaji wa haki za binadamu au za watu, itatoa amri zinazofaa ili kusuluhisha ukiukaji huo, ikiwa ni pamoja na malipo mazuri ya fidia.

Kuhusiana na hasara ya kimaadili, Mahakama ilirejelea kwamba ilikuwa imekiuka haki ya kuishi na haki ya utu kwa matendo ya kinyama na udhalilishaji. Mahakama iliendelea kuona kwamba ingawa hukumu ya kifo ilikuwa bado haijatekelezwa, Mleta Maombi alikuwa ameathiriwa na ukiukaji uliofanywa uliosababishwa na kutolewa kwa hukumu ya kifo ya lazima. Kwa hivyo ilimpa Mleta Maombi kiasi cha Shilingi Laki Tatu za Tanzania (TZS 300,000) kama fidia ya hasara ya kimaadili, kwa kuzingatia utoaji wa fidia kama hizo zinazohusisha Mjibu Maombi.

Kuhusu fidia zisizo za kifedha, Mahakama , ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi ya kuachiliwa huru; ilimwamuru Mjibu Maombi afute hukumu ya kifo aliyopewa Mleta Maombi na kumwondoa kwenye hukumu ya kifo; ilimwamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu kuondoa adhabu ya kifo ya lazima kwenye sheria zake ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya Hukumu hii; ilimwamuru Mjibu Maombi achukue

hatua zote muhimu ndani ya mwaka mmoja baada ya kupokea taarifa ya Hukumu hii, kwa ajili ya kupitia upya kesi kuhusu kutoa hukumu kwa Mleta Maombi kupitia utaratibu ambao hauruhusu kutoa hukumu ya kifo kwa lazima na ambayo inampa afisa wa mahakama uhuru wa uamuzi; na iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya Hukumu hii ili kuondoa adhabu ya "kunyongwa" kutoka kwenye sheria zake kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo.

Aidha, Mahakama, iliamuru Mjibu Maombi achapishe hukumu hii, ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa, kwenye tovuti za Mahakama, na Wizara ya Katiba na Sheria, na kuhakikisha kuwa hati ya hukumu inapatikana kwa angalau mwaka mmoja baada ya tarehe ya kuchapishwa. Mjibu Maombi aliamriwa, ndani ya miezi sita tangu tarehe ya taarifa ya hukumu hii kutolewa, awasilishe ripoti kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo yake na baada ya hapo, kila baada ya miezi sita hadi Mahakama itakapoona kuwa kumekuwa na utekelezaji kamili.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

## Maelezo Zaidi

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0152018

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org